



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI  
ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE



*Unapojibu tafadhali taja*

Kumb Na. TMC/MD/E.5/1/66

Tarehe: 01/07/2022

### **NAFASI ZA KAZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa Fedha 2021/ 2022 yenye Kumb. Na. FA/170/374/01"A"/ 16 cha tarehe 15 Juni, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi iliyoainishwa katika tangazo hili, kama ifuatavyo:

#### **1.1 DEREVA DARAJA LA II ( NAFASI 2)**

#### **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

- I. Awe amefaulu kidato cha nne (IV)
- II. Leseni ya daraja E au C<sub>1</sub> ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali
- III. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na Serikali
- IV. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

#### **MAJUKUMU YA KAZI YA UDEREVA**

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari

- Kufanya usafi wa gari na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

### **NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara ya Serikali, yaani TGS B kwa mwezi.

### **MASHARTI KWA UJUMLA**

- Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri usipungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka orobaini ni tano (45)
- Mwombaji ambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatishe maelezo yao binafsi (C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha moja ya rangi katika barua ya maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyaovinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya RESULT SLIP) HAVITAKUBALIWA
- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika waachukuliwa hatua za kisheria
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe


### **MAOMBI YATUMWE KWA ANWANI IFUATAYO:-**

MKURUGENZI WA MANISPAA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE,  
S.L.P 46343,  
**DAR ES SALAAM.**

Tangazo hili linapatikana pia katika wavuti ya Manispaa ([www.temekemc.go.tz](http://www.temekemc.go.tz)) na wavuti wa Serikali ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta, mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Jumanne tarehe 14/7/2022 saa 9.30 Alasiri.

Imetolewa na

  
Elihuruma Mabela  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**

MKURUGENZI WA MANISPAA  
TEMEKE



**Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022**